JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

# HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA e-GA KWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. JENISTA MHAGAMA (MB), WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA 3 CHA SERIKALI MTANDAO (e-GA) FEBRUARI 10, 2023 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.

---

*Mhe. Jenista Mhagama (Mb); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Mhe. Felician Mtahengerwa; Mkuu wa Wilaya ya Arusha,*

*Mhe. Xavier Daudi; Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Dkt. Jasmin Bunga, Makamu Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

*Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika naTaasisi Mbalimbali,*

*Wakuu wa Idara za Tehama na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

*Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

*Waandishi wa habari;*

*Mabibi na Mabwana;*

*Itifaki imezingatiwa;*

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka pamoja kwa kipindi chote cha siku hizi tatu (3) ikiwa leo ndiyo tamati ya Kikao Kazi hiki cha Tatu (3) cha Serikali Mtandao.

Kwa niaba ya menejimenti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), nawashukuru washiriki wote wa Kikao Kazi hiki kilichotukutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao nchini, na kupata fursa ya kujadiliana kuhusu jitihada mbalimbali za kukuza Serikali Mtandao, pamoja na kushauriana juu ya namna bora ya kukabiliana na changamoto tunazokutana nazo katika utekelezaji wa Majukumu yetu kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Aidha, niwapongeze na kuwashukuru kwa umakini, utulivu na usikivu wenu wakati wote wa Kikao kazi hiki, lakini pia niwashukuru kwa michango mliyotoa, ambayo imelenga katika kufanikisha na kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa ajili ya

kuboresha utendaji kazi wa Taasisi zetu, pamoja na utoaji wa huduma kwa umma.

**Mhe. Waziri;** Katika kipindi cha siku tatu za kikao kazi hiki, jumla ya washiriki 1624 wamehudhuria kikao hiki na mada 22 zilizolenga kutathmini na kuimarisha nguzo kuu Nne (4) za Serikali Mtandao ziliwasilishwa na wadau wetu kutoka katika taasisi mbalimbali za Umma. Mada hizo zilihusu namna ambavyo Taasisi hizo zimekuwa zikitekeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

**Mhe. Waziri,** Taasisi zilizowasilisha mada hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknlojia ya Habari, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Maji, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Tume ya TEHAMA (ICTC), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

**Mhe. Waziri,** kupitia mada hizo, washiriki walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata majibu pamoja na ufafanuzi wa hoja walizowasilisha wakati wa majadiliano. Naimani kuwa, kikao hiki kimewajengea uwezo zaidi washiriki kuhusu Serikali Mtandao na kila mtumishi ametambua namna ambavyo anawezakufanikisha jitihada za Serikali Mtandao kupitia sekta yake.

**Mhe. Waziri;** kutokana na nafasi waliyonayo Watendaji wakuu wa Taasisi (Maafisa Masuuli) katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, kupitia kikao kazi hiki Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ilifanya kikao maalum na viongozi hao na kujadiliana nao kwa pamoja kuhusu mikakati mbalimbali ya kukuza jitihada za Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Mamlaka.

**Mhe. Waziri,** pamoja na uwasilishaji wa mada na majadiliano, washiriki walipatiwa historia pamoja na hatua za ukuaji wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini, ambayo ilishika kasi zaidi baada ya kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao Mwaka 2012 na hatimaye kufanya mapinduzi makubwa ndani ya kipindi cha miaka kumi (10).

**Mhe. Waziri,** Vilevile washiriki wametoa maoni mbalimbali ya namna ya kukuza jitihada za Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na kushauri uboreshaji wa Mifumo mbalimbali inayotoa huduma kwa

umma pamoja na kupanua wigo wa utoaji wa huduma za Serikali Mtandao katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mhe. Waziri;** Napenda kuwathibitishia washiriki wa kikao kazi hiki kuwa, Menejimenti ya Mamlaka imeyapokea maoni na ushauri uliotolewa hapa, ambao kwa ujumla umelenga kuboresha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini. Pia, Mamlaka ipo tayari kutekeleza maelekezo yako utakayotoa hapa leo.

**Mhe. Waziri,** kabla sijahitimisha naomba kuwatambua wadhamini wetu 28 ambao wamechangia kufanikisha kikao hiki kama ifuatavyo;-

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
2. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)
3. Azam Media Ltd.
4. Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA)
5. Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
6. Benki Kuu ya Tanzania (BOT)
7. SoftNET
8. NMB
9. UBX limited
10. Shirika la Bima la Taifa (NIC)
11. Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania (ERB)

12. CRDB
13. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)
14. Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)
15. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (**NCAA**)
16. Tanzania National Parks (TANAPA)
17. Tanzania Comercial Bank (TCB)
18. Mamlaka ya Dawa na vifaa tiba (TMDA)
19. INFOGEAR
20. Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (**DART**),
21. Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL)
22. ICT Comission
23. Technology Associate
24. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
25. Watumishi Housing Investment (WHI)
26. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)
27. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)
28. Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)

Mwisho kabisa, nirudie tena kukushuru wewe **Mhe. Waziri** pamoja na washiriki wote mliohudhuria Kikao Kazi hiki, pamoja na kuomba

utayari wenu pindi tutakapowaalika katika kikao kingine kama hiki wakati mwengine.

*Asanteni sana kwa kunisikiliza*